BILA MAOMBI MENGI, utachezewa sana, utatapeliwa sana, utapigika sana, utahangaishwa sana na mwishowe utalishwa na kunyweshwa vichafu vingi na kuambiwa kuwa ndio upako au ufunuo.

Imeandikwa kuwa nyumba yangu itakuwa ni nyumba ya sala LUKA 19:46, 1 FALM. 8:33-40, 2 NYAKATI 20:9); ***Je inatumika kwa sala kweli? kwani;***

Vita vyetu si juu ya damu na nyama, Bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. WAEFESO 6:11-12 2KOR. 10:3-5

TUMIA KITABU HIKI KULIOKOA KANISA LA MUNGU, NA PIA KITUMIE KUONGEA NA MMEO/MKEO AU FAMILIA YAKO KWA UJUMLA KWA KUMSISITIZIA ASOME MARA KWA MARA NA KWA KUMFAFANULIA MARA KWA MARA UNAYOYAELEWA KUHUSIANA NA MAOMBI MENGI ILI KUMTOA KATIKA MIKONO YA SHETANI.

Na Mbarikiwa Mwakipesile

© Mbarikiwa Mwakipesile, 2015

Simu: 0769015164
Barua pepe: mbarikiwamwakipesile@gmail.com
Mbeya
Tanzania
ISBN-978-9987-749-42-3.

YALIYOMO

MAOMBI YANGU..... i
DIBAJI..... ii
UTANGULIZI..... iv
Sura ya Kwanza..... 1
NGUVU ILIYOJIFICHA KATIKA MAOMBI MENGI..... 1
Sura ya pili..... 15
MAOMBI MENGI HUTUFANYA TUWE NA SHABAHA YA MAMBO MENGI/YOTE TUYAFANYAYO..... 15
Sura ya Tatu..... 21
NUKUU YA BAADHI YA MAHUBIRI YALIYOHUBIRIWA "LIVE" KUTOKA KATIKA IBADA ZETU..... 21
Sura ya Nne..... 29
MAOMBI MENGI NI NINI?..... 29
Sura ya Tano..... 33
TUNAPOKEAJE MAJIBU BAADA/WAKATI WA KUOMBA?..... 33
Sura ya sita..... 43
JE INAWEZEKANA KUKOSA MAJIBU KWA SABABU NIMEOMBA VIBAYA? KUOMBA VIBAYA NI NINI?..... 43
Sura ya Saba..... 53
CHANGAMOTO TUNAZOKUTANA NAZO TUNAPOKUWA KATIKA MAOMBI MENGI..... 53
Sura ya Nane..... 61
KWA NINI TUOMBE KWA DAKIKA NYINGI WAKATI WA IBADA ZETU? 61
Sura ya Tisa..... 67
NI WAKATI GANI HASA UFAAO KUOMBA?..... 67
Suraya Kumi..... 69
JE KUNA UHUSIANO WOWOTE KATI YA MAOMBI MENGI NA KUFUNGA KWINGI?..... 69
Sura ya kumi na moja..... 73
JE KUNA UWEZEKANO WA KULIA UNAPOOMBA? NA JE KUNA SABABU ZA KULIA UNAPOOMBA?..... 73

Sura ya kumi na mbili 77
KUNA UHUSIANO WOWOTE WA KUOMBA NA KUNENA KWA LUGHA? KUNENA KWA LUGHA NINI? 77
Sura ya kumi na tatu 81
JE KUNA SABABU YA KUOMBA MAOMBI MENGI HATA KAMA NIKO CHINI YA MCHUNGAJI ANAYEKESHA KWA AJILI YANGU? 81
Sura ya kumi na nne 87
KUNA SABABU YOYOTE YA KUWA NA MAOMBI MENGI IKIWA NINA ROHO MTAKATIFU? 87
Sura ya kumi na tano 91
KUNA TOFAUTI YOYOTE KATI YA KUOMBA NA KUKEMEA? 91
Sura ya kumi na sita 95
JE, KUNA MADHARA YOYOTE YA KUOMBA NA KUACHA? 95
Sura ya kumi na saba 99
NIFANYE NINI ILI NIWEZE KUOMBA MAOMBI MENGI? 99
Sura ya kumi na nane 103
SABABU YOYOTE ITAKAYOKUFANYA USHINDWE KUWA NA MAOMBI MENGI NDIYO MACHINJIO YAKO YA KUCHINJIA NA KUCHINJIWA 103
Sura ya kumi ta tisa 109
ASANTE MUHUBIRI KWA MAFUNDISHO YAKO HAYA YAHUSUYO MAOMBI MENGI NA KWA SABABU HIYO MIMI NIMEKUBALI NA NIMEANZA KUWA NA MAOMBI MENGI, ILA NITAOMBA HADI LINI? AU NITAACHA KUOMBA BAADA YA KUONA NINI? 109
Sura ya ishirini 111
MAPENDEKEZO YANGU 111
Sura ya ishirini na moja 115
MSIMAMO WANGU 115
Sura ya ishirini na mbili 117
BAADHI YA SHUHUDA ZA WATU MBALIMBALI BAADA YA KUANZA KUWA NA MAOMBI MENGI 117
Sura ya ishirini na tatu 120
KUHUSU MWANDISHI 120

MAOMBI YANGU

Namuomba Mungu kwamba kila aliyeokoka au aliyeingia kanisani kwa kusudi la kumtafuta Mungu aweze kusoma kitabu hiki. Lakini Pia namuomba Mungu kitabu hiki kisomwe na wahubiri wote wanaohubiri kwa ajili ya maslahi ya Mungu na hata wakitumie kuwaimarishia watu wao. **Kwani watu wao/wa Mungu wakifahamu jinsi ya kuwa na maombi mengi, watapata ufunguo wa kila kufuli, komeo, kitasa au pingu iliyofunga maisha yao kwa namna yoyote.**

Lakini pia ni maombi yangu kuliombea kanisa kote duniani ili watambue kuwa; kanisa lolote au mtu yeyote aliye na uwezo wa kutoa mapepo au kupona magonjwa kokote kunakotokana na maombezi, kama tu kanisa hilo au mtu huyo hana maombi mengi yaliyo zaidi ya haya yaliyopendekezwa katika kitabu hiki; Basi KINACHOFANYIKA HAPO NI MAZINGAOMBWE NA VIINI MACHO.

Na ili uthibitishe kuwa ni viini macho, basi watu wote wanaoombewa hapo hurudiwa na mateso yale yale na hata zaidi ya yale na huwa WANAKUWA NA MAISHA MACHAFU SANA (YA KALE) na huwa hawadumu siku nyingi katika wokovu.

Lakini pia namuomba Mungu akujulishe na kukufunulia ukweli uliomo katika maombi mengi ambapo pasipo maombi mengi, mguso wowote unaokuwepo kwenye ibada, au kushangilia kokote kunakokuwepo wakati wa ibada au sherehe au kufaulu masomo, kupata kazi au faida kubwa katika biashara au kilimo**, HAKUTAKUWA NA RAHA AU FURAHA ITAKAYODUMU. Ghafla utajikuta kwenye maumivu makali ya moyo, mwili au ufahamu bila kujua chanzo chake na huku ukiwa huna nguvu ya kuirudisha hali ya furaha uliyokuwa nayo hata kama vitu hivyo vitakuwepo au kuongezeka.**

Bwana na akupe kuyaelewa maneno yaliyoandikwa katika kitabu hiki na MUNGU NA AWE JUU YA MANENO HAYA, KATIKA JINA LA YESU KRISTO, AMENI.

DIBAJI

Kitabu hiki ni majibu ya maswali mengi waliyonayo watu kuhusu maombi. Na ndio maana katika maeneo mengi kimeandikwa kwa mfumo wa maswali na majibu. Ni kitabu tunachoamini kuwa kila ukurasa au aya au kichwa cha somo utakachokisoma, kitakufanya uanze kupenda kuomba sana. Ni kitabu tunachoamini kuwa aweza kukisoma mtu wa aina yoyote na akakielewa. Chaweza kutumika kuwaimarisha watoto wachanga katika wokovu, lakini pia chaweza kuwaimarisha waliodumu siku nyingi katika wokovu, **lakini pia chaweza kumfanya kiongozi/muhubiri aongoze/ahubiri kwa sura ambayo hajakuwa nayo hapo kabla kwa sababu ya uwezo uliomo katika maombi atakayoomba baada ya kusukumwa au kuhamasishwa au kuhimizwa na kitabu hiki, kwa namna moja au nyingine.**

Tunapenda usome kitabu hiki ukiwa katika kila jitihada ya kutaka kuomba sana, kwani ndipo utakielewa sana na **baada ya hapo utaitazama dunia kwa namna ambayo hujawai kuiona hivyo.** Utaona dunia ikikusujudia nawe ukiwa juu ya kila kilichoumbwa bila hata ya kutumia nguvu kubwa au bila hata ya kutabiriwa. Ni "automatic" unaanza kujiona kuwa wewe si yule wa zamani.

Mimi niliyeandika kitabu hiki ni mshirika wa baraka hii na ndio maana natumia kila aina ya mbinu na uwezo wangu ili nikushirikishe baraka hii. Mimi kwangu maombi ni ufunguo wa kila kitasa/kufuli. Yako mambo hayakuwa na ufumbuzi wake toka nizaliwe, lakini baada ya kuujua ukweli huu, yako sawa sawa. Kuna usemi ambao watu husema; elimu ni ufunguo wa maisha au elimu ni ukombozi. Lakini si hivyo kwangu; mimi elimu iliniacha nikiwa "hohehahe" na wenzangu wote niliowaacha katika elimu hiyo (walioikataa baraka hii ya maombi mengi) leo hii wengi wao wamechakaa sana na wengine ni marehemu.

Na pia kuna usemi mwingine unasema; pesa ni jawabu la mambo yote. Mimi kwangu maombi ndiyo jawabu la mambo yote. Kwani nimefahamu kuwa elimu, au pesa, ni ufunguo au jawabu la mambo "baadhi" Lazima mtu huyu mwenye elimu au mali, pembeni yake awe na maombi mengi. Vinginevyo huonyesha kwa nje tu kuwa ana furaha au amani. Lakini uhalisia wa maisha yake, ni matatizo na mahangaiko mengi sana katika moyo wake na mwili wake.

Mimi nimetambua na nimehakikisha kuwa ukilifundisha kanisa au mtu kuhusu kuomba na akaanza kuomba sana pamoja na kujituma katika kazi zake, hautapata taabu ya kumfundisha au kumsukuma kwa lingine lolote. Huwezi tena kutafuta kila aina ya mbinu na kutafuta aina nyingi ya maandiko ili kumfanya mtu atoe "fedha kubwa kubwa", aache kuchelewa ibada, asiwe mvivu wa ibada, ama kuacha aina fulani ya ubaya. "Automatic" mtu akianza kuwa na maombi mengi, hujikuta akijisukuma mwenyewe kwa mambo mengi sana.

Wakati fulani nilipokuwa kanisani nilisema kuwa; sitaacha kuhubiri fundisho hili (linalohusu maombi mengi) mpaka umeanza kuomba sana na umeona faida zake. Maombi mengi ndiyo yanayotifua udongo (wa mioyo) na kuuweka tayari kwa kila mbegu njema. Narudia tena hata kwako; NITAHUBIRI MAOMBI MENGI MPAKA UTAKAPOANZA KUOMBA SANA NA KUONA FAIDA ZAKE. Lakini napo sitaacha kabisa ila nitakukumbusha walau mara mbili kwa kila juma lakini kwa sasa natamani kila ninapokuona nizungumzie maombi.

Imeandikwa kuwa nyumba yangu itakuwa ni ya sala (LUKA 19:46, 1 FALM. 8:33-40, 1 NYAKATI 20:9); Mbona imekuwa ni ajabu kuwakuta watu usiku au mchana wakiomba?

UTANGULIZI

Bila maombi mengi, haijalishi una gari au hauna, Umeolewa au haujaolewa, una nyumba au hauna, una pesa au hauna. **Katika hali yoyote uliyonayo (bila maombi mengi), dunia hii "itakukimbiza sana"**. Hata uchekeje baada ya kupanda cheo, kupata mtoto wa kike au kiume, kufaulu masomo, kupata faida kubwa katika biashara yako au mashamba yako, ama kupata kazi, bado utakimbia mchaka-mchaka wa kukutosha. Kila simu utakayopokea hutaamini kuwa ni salama mpaka umesikiliza kilichoongelewa. Utakuwa na muda mwingi wa moyo kwenda mbio. Na utajifariji kuwa wanadamu wote tuko hivi na kumbe ni wewe tu na mwenzio huyo asiyependa maombi kama wewe. **Bila maombi mengi dunia inawaka moto**, ni mchakamchaka wa rohoni na mwilini mpaka unakufa. Na mchakamchaka huo nimekuambia kuwa hauogopi chochote ulichonacho au unachokitamani. Kama kuna mtu unamuona ana furaha kwa sababu ya chochote unachokitamani we jua kuwa yale ni maigizo tu, yale ni madoido tu, zile ni mbwembwe tu, ukweli wa hali ya moyo wake ni "vidonda vitupu". Anacheka kwa kumuona, lakini usiku, au akiwa peke yake anakimbizwa vya kutosha.

Dunia hii iliyojaa kuviziwa, kuwindwa, kuonewa wivu, kuchokozwa kwingi, kuandamwa kwa wanaotaka kuishi kwa haki, kuvunjwa moyo na kuumizwa na kila unalosikia, unaloliona au kuhisi, n.k, BILA MAOMBI MENGI utakuwa ni "mgonjwa wa moyo au mwili mpaka unakufa". Ama utakuwa na kipindi kirefu cha kujisikia vibaya kuliko kujisikia vizuri. Wewe kwako duniani patakuwa pamoto. Kila kukicha itakuwa afadhali ya jana**, wakati mwenye maombi mengi kila kunapokucha ni afadhali ya leo.**

Bila kujalisha kazi yako, muda wako, jinsia yako, umri wako, nafasi uliyonayo katika jamii au kanisani, fanya kila uwezalo ili uwe ni mwenye maombi mengi. Vinginevyo; **utachezewa sana**, utatapeliwa sana, utaibiwa sana na utanyanyaswa sana katika dunia hii.